

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR



**Taarifa ya Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Mhe. Jecha Salim Jecha Katika
Mkutano na Waandishi wa Habari Juu ya Mabadiliko ya Idadi, Mipaka na
Majina ya Majimbo ya Uchaguzi ya Zanzibar**

Tarehe 6 Julai, 2015

Hoteli ya Grand Palace Malindi

Wawakilishi wa Vyombo vya Habari;

Viongozi wa Asasi za Kijamii;

Mabibi na Mabwana.

Assalam Aleykum

Kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tukiwa wazima na wenye afya. Kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi natoa shukurani nyingi kwa kukusanyika nasi muda huu ili kusikiliza taarifa muhimu tutakayoiwasilisha kwa wananchi na wadau wa uchaguzi kupitia katika vyombo mbalimbali mnavyoviwakilisha.

Katika mkusanyiko wa leo tutaitoa taarifa hiyo, lakini naomba muwe na subira kidogo na msikilize maelezo mafupi juu ya chanzo cha kazi hii na katika kuifanya kazi hii ni mambo gani muhimu yaliyozingatiwa na Tume

Ndugu Waandishi, Katiba ya Zanzibar, 1984, Kifungu cha 120(4), kinaiielekeza, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuwa katika kipindi cha miaka 8 hadi 10 au wakati mwengine wowote, kuchunguza idadi ya mipaka na majimbo ya uchaguzi na baada ya uchunguzi wake inaweza kubadili idadi, mipaka na majina ya majimbo hayo.

Ndugu Waandishi, kwa kuzingatia maelekezo hayo ya kisheria na kwa kuwa ilikuwa tayari inakaribia miaka 10 tangu mapitio ya mwisho ya majimbo ya uchaguzi yalipofanyika (2004), na kwa kuwa kuacha kuitekeleza kazi hizo, Tume ingekuwa inakiuka Katiba ya Zanzibar, Juni 2014 Tume iliandaa Mpangokazi wa kazi ya

uchunguzi wa majimbo na iliusambaza mpango kazi huo kwa Wadau mbalimbali vikiwemo vyama vya siasa.

Mpangokazi huo ulikuwa na maeneo manane ambayo yalipangwa kutekelezwa na Tume katika kazi hiyo. Maeneo hayo ni utoaji wa taarifa kwa wadau juu ya kazi ya uchunguzi wa majimbo na kupitia vyombo vya habari na mikutano na wadau tuliwajulisha wananchi juu ya kazi hiyo muhimu.

Eneo jengine lilikuwa ni kupokea maoni ya vyama vya siasa. Katika kazi hii, Tume ilikutana ana kwa ana na Wawakilishi wa vyama 18 vya siasa vyama vinne vilituma maoni yao kwa maandishi. Aidha, Tume ilipokea maoni kutoka Taasisi za Serikali ambapo katika utaratibu huu tulikutana na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, tulikutana na Wawakilishi wa Wizara zote zinazohusika na masuala ya Utawala Bora, masuala ya Tawala za Mikoa, Jeshi la Polisi. Vile vile, tulikutana na Viongozi wa kuchaguliwa kama vile vile Wawakilishi, Wabunge na Madiwani wote wa Unguja na Pemba na hatimae tulifanya mikutano ya wazi ya upokeaji wa maoni ya wananchi na Asasi za kijamii kwa Wilaya zote.

Ndugu Waandishi, baada ya mikutano yote hiyo na wadau tulifanya ziara za kutembelea maeneo ya mipaka ya Shehia yaliyolalamikiwa wakati wa kupokea maoni pamoja na kuwa maeneo hayo yako chini ya mamlaka nyengine, tulitembelea mipaka ya wadi na majimbo yote yaliyokuwa yanaguswa sana wakati wa kupokea maoni. Tume ililazimika kutembelea maeneo yote yaliyolalamikiwa nchi nzima, ili kuona maeneo ya mipaka ya majimbo na wadi yaliyolalamikiwa wakati wa upokeaji wa maoni na hatimae kufanya uchambuzi wa maoni yote.

Uchambuzi wa maoni yaliyopokelewa ulifanyika kwa kuzingatia maelekezo ya Katiba, Kifungu cha 120(3) kinasomeka kuwa ; majimbo yote yatakuwa karibuni na wakaazi sawasawa kama inavyoonekana na Tume, lakini Tume inaweza kuepuka shuruti hii kwa kiwango kile kinachofikiria kuwa inafaa kwa ajili ya kuzingatia

- i. idadi ya watu na zaidi katika kuhakikisha uwakilishi unaofaa katika miji mikubwa na miji ya mashamba yenye idadi ndogo ya watu;
- ii. ukuaji wa idadi ya watu;
- iii. njia za usafiri; na
- iv. mipaka ya sehemu ya utawala.

Ndugu Waandishi kutokana na maoni ya wadau, ziara ambazo tulizifanya katika maeneo mbalimbali na takwimu zinazohusiana na watu na makaazi, Tume ilishawishika kuwa kuna ongezeko kubwa la idadi ya watu katika baadhi ya majimbo na eneo lililozidiwa sana ni Wilaya ya Magharibi.

Eneo hilo limeonyesha kuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu kulinganisha na eneo jengine lolote lile la Zanzibar. Lakini kwa kutumia vigezo hivyo hivyo, Tume ilibaini kuwa kuna baadhi ya majimbo ambayo yana idadi ndogo sana ya watu.

Kufuatia matokeo hayo ya uchunguzi, Tume ilikubaliana kuwa kuna haja kubwa ya kufanya marekebisho ya idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi kwa kuzingatia maelekezo ya Sheria yanayoelekeza kuwepo na uwiano wa watu baina ya jimbo na jimbo.

Ndugu Waandishi, Tume tayari imekamilisha taarifa ya kazi ya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo na iko tayari kuitangaza rasmi mipaka mipya ya majimbo ya uchaguzi kwa umma. Kazi hii kwa asilimia mia kubwa sana imefanywa kwa kuzingatia maoni ya wadau wote. Tume ya Uchaguzi imeongeza idadi ya majimbo ya Uchaguzi na hivyo kupelekea mabadiliko makubwa ya mipaka ya majimbo kwa takriban majimbo yote. Mabadiliko hayo yatapelekea baadhi ya majina ya majimbo kubadilika.

Ndugu Waandishi Tume ya Uchaguzi inapenda kutoa taarifa kuwa imekamilisha kazi yake ya uchunguzi wa Idadi, Mipaka na Majina ya majimbo ya Uchaguzi. Tume imeongeza idadi ya majimbo manne ya uchaguzi ya Wawakilishi na kufanya jumla majimbo yote kuwa 54 badala ya 50 yalokuwa ya awali. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwatangazie majimbo ya uchaguzi yatakayotumika katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Mkoa wa Kaskazini Pemba (Majimbo Tisa)

WILAYA YA MICHEWENI (4)		
JIMBO	N	SHEHIA
Konde	1	Kifundi
	2	Konde
	3	Kipange (P)
	4	Makangale
	5	Tondooni
	6	Msuka Mashariki
	7	Msuka Magharibi
Micheweni	1	Kiuyu Mbuyuni
	2	Shanake
	3	Maziwa Ng'ombe
	4	Majenzi
	5	Micheweni
	6	Chamboni
	7	Shumba Mjini
Tumbe	1	Tumbe Mashariki
	2	Tumbe Magharibi
	3	Mihogoni
	4	Shumba Viamboni
	5	Kinowe
	6	Chimba
Wingwi	1	Mjini Wingwi
	2	Sizini
	3	Wingwi Mapofu
	4	Wingwi Njuguni
	5	Mtemani

WILAYA YA WETE (5)		
JIMBO	N	SHEHIA
Gando	1	Gando
	2	Junguni
	3	Ukunjwi
	4	Fundo
	5	Bopwe
	6	Kizimbani
Kojani	1	Chwale
	2	Mpambani
	3	Kojani
	4	Kinyikani
	5	Mchanga Mdogo
	6	Kangagani
	7	Kiuyu Kigongoni
	8	Kiuyu Minungwini
	9	Kambini
	10	Shengejuu
Mtambwe	1	Kisiwani
	2	Mtambwe Kusini
	3	Mtambwe Kaskazini
	4	Piki
	5	Mzambarau Takao
	6	Maziwani
Mgogoni	1	Pandani
	2	Mgogoni
	3	Finya
	4	Kinyasini
	5	Mjananza
	6	Kiungoni
	7	Pembeni
	8	Mlindo
Wete	1	Selem
	2	Jadida
	3	Mtemani
	4	Kipangani
	5	Limbani
	6	Utaani

Mkoa wa Kusini Pemba (Majimbo Tisa)

WILAYA YA CHAKECHAKE (5)		
JIMBO	N	SHEHIA
Chake Chake	1	Madungu
	2	Chanjaani
	3	Shungi
	4	Kichungwani
	5	Tibirinzi
	6	Chachani
	7	Msingini
Chonga	1	Chonga
	2	Kilindi
	3	Mgelema
	4	Matale
	5	Mfikiwa
	6	Pujini
Ole	1	Mjini Ole
	2	Ole
	3	Mchanga Mrima
	4	Ng'ambwa
	5	Uwandani
	6	Vitongoji
Wawi	1	Kibokoni
	2	Gombani
	3	Mvumoni
	4	Mgogoni
	5	Mkoroshoni
	6	Wara
	7	Wawi
Ziwani	1	Ziwani
	2	Kwale
	3	Mbuzini
	4	Ndagoni
	5	Michungwani
	6	Wesha

WILAYA YA MKOANI (4)		
JIMBO	N	SHEHIA
Chambani	1	Ngwachani
	2	Chambani
	3	Dodo
	4	Wambaa
	5	Chumbageni
	6	Mgagadu
	7	Ukutini
Kiwani	1	Jombwe
	2	Kiwani
	3	Kendwa
	4	Mtangani
	5	Kengeja
	6	Chole
	7	Muambe
	8	Shamiani
Mkoani	1	Chokocho
	2	Mkanyageni
	3	Kisiwa Panza
	4	Michenzani
	5	Stahabu
	6	Makoongwe
	7	Mbuyuni
	8	Shidi
	9	Makombeni
	10	Ng'ombeni
	11	Uweleni
	12	Mbuguani
	13	Changaweni
Mtambile	1	Kangani
	2	Kengeja/Mchakwe
	3	Kuukuu
	4	Mkungu
	5	Minazini
	6	Mizingani
	7	Mjimbini
	8	Mtambile

Mkoa wa Kaskazini Unguja (Majimbo Tisa)

WILAYA YA KASKAZINI "A" (5)		
JIMBO	N	SHEHIA
Chaani	1	Kinyasini
	2	Kikobweni
	3	Kandwi
	4	Pwani Mchangani
	5	Mchenza Shauri
	6	Chaani Kubwa
	7	Chaani Masingini
	8	Bandamaji
Kijini	1	Kigongoni
	2	Potoa
	3	Kijini Matemwe
	4	Mbuyutende
	5	Kigomani
	6	Juga Kuu
	7	Kivunge
	8	Pitanazako
	9	Muwange
Mkwajuni	1	Matemwe Kaskazini
	2	Matemwe Kusini
	3	Kibeni
	4	Kidombo
	5	Chutama
	6	Gamba
	7	Moga
	8	Mkwajuni
Nungwi	1	Nungwi
	2	Kiungani
	3	Kilindi
	4	Bwereu
	5	Kidoti
	6	Kilimani Tazari
	7	Tazari
	8	Fukuchani
	9	Kigunda
Tumbatu	1	Kipange
	2	Mchangani
	3	Muwanda
	4	Mkokotoni
	5	Mto wa Pwani
	6	Pale
	7	Mtakuja
	8	Gomani
	9	Uvivini
	10	Jongowe

WILAYA YA KASKAZINI "B" (4)		
JIMBO	N	SHEHIA
Bumbwini	1	Misufini
	2	Kidanzini
	3	Makoba
	4	Mafufuni
	5	Kiongwe Kidogo
Donge	1	Donge Mtambile
	2	Majenzi
	3	Njia ya Mtoni
	4	Donge Vijibweni
	5	Donge Karange
	6	Donge Pwani
	7	Donge Mbiji
	8	Mnyimbi
	9	Mkataleni
Kiwengwa	1	Kiwengwa
	2	Upenja
	3	Pangeni
	4	Kisongoni
	5	Mgambo
	6	Kitope Kwagube
	7	Mbaleni
	8	Kilombero
Mahonda	1	Mangapwani
	2	Fujoni
	3	Kiombamvua
	4	Kitope
	5	Mkadini
	6	Zingwezingwe
	7	Kinduni
	8	Mahonda
	9	Matetema

Mkoa wa Kusini Unguja (Majimbo Matano)

WILAYA YA KATI (3)		
JIMBO	N	SHEHIA
Chwaka	1	Ukongoroni
	2	Charawe
	3	Pete
	4	Cheju
	5	Ndijani Mseweni
	6	Ndijani Mwembepunda
	7	Jendele
	8	Chwaka
	9	Marumbi
	10	Uroa
	11	Pongwe
Tunguu	1	Jumbi
	2	Binguni
	3	Tunguu
	4	Dunga Bweni
	5	Dunga Kiembeni
	6	Ubago
	7	Bungi
	8	Kikungwi
	9	Ng'ambwa
	10	Tindini
	11	Unguja Ukuu Kaebona
	12	Unguja Ukuu Kaepwani
	13	Uzi
Uzini	1	Ghana
	2	Kiboje Mkwajuni
	3	Kiboje Mwembeshauri
	4	Tunduni
	5	Mitakawani
	6	Uzini
	7	Mgeni Haji
	8	Kidimni
	9	Koani
	10	Machui
	11	Miwani
	12	Bambi
	13	Mchangani Shamba
	14	Mpapa
	15	Pagali
	16	Umbuji

WILAYA YA KUSINI (2)		
JIMBO	N	SHEHIA
Paje	1	Michamvi
	2	Dongwe
	3	Bwejuu
	4	Paje
	5	Jambiani Kibigija
	6	Jambiani Kikadini
	7	Kitogani
	8	Muungoni
Makunduchi	1	Kajengwa
	2	Nganani
	3	Kiongoni
	4	Kijini
	5	Tasani
	6	Mzuri
	7	Muyuni 'A'
	8	Muyuni 'B'
	9	Muyuni 'C'
	10	Kizimkazi Dimbani
	11	Kizimkazi Mkunguni
	12	Kibuteni
	13	Mtende

Mkoa wa Mjini Magharibi (Majimbo Ishirini na mbili)

WILAYA YA MJINI (9)		
JIMBO	N	SHEHIA
Amani	1	Amani
	2	Kwa Wazee
	3	Kilimahewa Juu
	4	Kilimahewa Bondeni
Chumbuni	1	Chumbuni
	2	Karakana
	3	Banko
	4	Masumbani
	5	Mwembemakumbi
	6	Maruhubi
Jang'ombe	1	Jang'ombe
	2	Urusi
	3	Kwaalinatu
	4	Kidongo Chekundu
	5	Matarumbeta
Kikwajuni	1	Miembeni
	2	Mwembeladu
	3	Rahaleo
	4	Muembemadema
	5	Mwembeshauri
	6	Kikwajuni Juu
	7	Kisimamajongoo
	8	Kikwajuni Bondeni
	9	Mnazimmoja
	10	Kisiwandui
Kwahani	1	Kwaalimsha
	2	Kwahani
	3	Mikunguni
	4	Makadara
	5	Muungano
	6	Sebleni

WILAYA YA MJINI		
JIMBO	N	SHEHIA
Shaurimoyo	1	Kwamtipura
	2	Mboriborini
	3	Mkele
	4	Mapinduzi
	5	Shaurimoyo
	6	Saateni
Magomeni	1	Magomeni
	2	Meya
	3	Nyerere
	4	Kwamtumwajeni
	5	Sogea
Malindi	1	Gulioni
	2	Mitiulaya
	3	Vikokotoni
	4	Mlandege
	5	Muembetanga
	6	Malindi
	7	Mkunazini
	8	Kiponda
	9	Shangani
	10	Mchangani Mjini
Mpendae	1	Kilimani
	2	Migombani
	3	Mpendae
	4	Kwabintiamrani

Mkoa wa Mjini Magharibi inaendelea

WILAYA YA MAGHARIBI "A" (6)		
JIMBO	N	SHEHIA
Mtoni	1	Kibweni
	2	Kwa Goa
	3	Mwanyanya
	4	Mtoni
	5	Sharifu Msa
Bububu	1	Kijichi
	2	Mbuzini
	3	Bububu
	4	Chemchem
	5	Dole
	6	Kizimbani
Mfenesini	1	Chuini
	2	Kihinani
	3	Kikaangoni
	4	Kama
	5	Mfenesini
	6	Mwakaje
	7	Bumbwisudi
Mto Pepo	1	Mto Pepo
	2	Munduli
	3	Mtoni Kidatu
	4	Mtoni Chemchem
Mwera	1	Kianga
	2	Masingini
	3	Mwera
	4	Muembemchomeke
Welezo	1	Mtofaani
	2	Michikichini
	3	Hawaii
	4	Welezo
	5	Uholanzi

WILAYA YA MAGHARIBI "B" (7)		
JIMBO	N	SHEHIA
Dimani	1	Fumba
	2	Bweleo
	3	Dimani
	4	Nyamanzi
	5	Kombeni
	6	Maungani
	7	Uwandani
	8	Kibondeni
Fuoni	1	Fuoni Kipungani
	2	Fuoni Migombani
	3	Mambosasa
	4	Chunga
Kiembesamaki		Kiembesamaki
	1	Mbweni
	2	Mombasa
	3	Michungwani
	4	Kwa Mchina
Chukwani	1	Chukwani
	2	Shakani
	3	Kisauni
	4	Tomondo
Mwanakwerekwe	1	Magogoni
	2	Jitimai
	3	Sokoni
	4	Mikarafuuni
	5	Mwanakwerekwe
Pangawe	1	Muembe Majogoo
	2	Mnarani
	3	Kinuni
	4	Pangawe
Kijitoupele	1	Melinne
	2	Taveta
	3	Uzi
	4	Kijitoupele

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza